say that, as far as expenditures are concerned, the allocation of the available resources is certainly constrained by the amount of revenue that is available and for that matter, it is sad to hear, although understandable, that hon. Members are complaining they have not had anything in their own particular constituencies. Let me put the records right there. If you have a policeman, a teacher, a chief or a DO in your constituency, or if you have anybody employed by the Government, then you have had a share of the Budget because the Budget includes Recurrent Expenditure and---

**Dr. Lwali-Oyondi:** On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. Is the Assistant Minister in order to mislead this House when the hon. Members have explained to him exactly that they want development in their areas, but not recurrent expenditure? Is he in order to mislead the House that people have got---

**The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula):** Order, Dr. Lwali-Oyondi! There is no hon. Member who has explained anything to this Assistant Minister. You explain to the House, not the Assistant Minister.

**The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah):** Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I was referring to those who have commented on a generality, but not on Development Expenditure. Let me, however, add that I would like to urge the new Kenya Revenue Authority and its officers to be very, very vigilant in the collection of revenue as authorised by Parliament. We will support them fully. It is only when they collect that revenue that we will be able, as a Government, to spend on the items that have been allocated for spending. At this juncture, let me add a very important point that included within the revenue as a Budget. These are sums that are expected to be received either by way of loans or grants from our development partners, or the donor community. It will, indeed, be a pity and derailing the Budget if any hon. Member of Parliament or any Kenyan were to speak to our development partners and say: "Just because KANU is the Government, do not give any loans or any money to the KANU Government." That would be derailing this Budget and development as far as this country is concerned. Let us fight one another and even disagree; let KANU *versus* whoever fight; but let us know that when it comes to matters relating to nationalism and Kenya, we should know that we are all Kenyans and it is your brother and sister who is going to suffer if you are an agent, organ or engine that is going to stop a donor or a development partner from giving us their funds. This is a very relevant point because some people talk---

**Mr. Shikuku:** On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. How long can we allow the hon. Member to go on misleading this House? It is, and it has been clearly stated by the donors that the reasons for their withholding the aid is because the Government is corrupt and against political changes. They are stealing the money.

**The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula):** Order, hon. Shikuku! That is not a point of order.

**The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah):** Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, hon. Shikuku is taking my time unfairly. Thank you for defending me.

Let me say it here, loud and clear that, it is incumbent upon all Kenyans to defend their motherland, Kenya, regardless of your views. If you do not support your motherland Kenya, you are an enemy of Kenya. It has become a habit that whenever we go to meet with the donors, you find certain members of the Kenyan community talking as if they are not Kenyans at all. That habit must stop. Let me say that the issue of corruption relates to financial discipline in the whole country. No one Government or Parliament can make rules that will stop corruption, unless we Kenyans are prepared, all of us together, to stop corruption, inclusive of KANU, Opposition and even those who belong to no political parties.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I repeat that, that includes KANU, Opposition and other people who do not belong to any party at all. It is important to note that wherever there is corruption, there are two people involved; the giver and the receiver. It is incumbent upon Kenyans to make sure that the culture of corruption is fought by us all to the very bitter end.

Let me now talk about Kaloleni Constituency. Water is very important; roads and electricity are very necessary. I would like to urge the Ministry of Land Reclamation, Regional and Water Development to make sure that a bigger portion of the Budget goes to the provision of water to the entire Republic. In Kaloleni Constituency, we have water shortage and I would---

**Mr. Shikuku:** On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. According to the rules of this House, is it in order for the Assistant Minister to speak the way he is speaking now? He is in the Government. Whom is he appealing to?

**The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah):** Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I am speaking to the officers in the Ministries; I am speaking to the country and I am speaking to the planners. I am speaking particularly to hon. Shikuku. He should not take my time because I want to put my points across. Hon. Shikuku ought to behave better than this. He has taken my time and it is not fair for him to do that.

**Mr. Shikuku:** On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. Is the hon. Member in order to continue speaking when I am on a point of order? I have been in the Government and I know that according to the

rules of this House, you cannot appeal to the Government when you are in the Government. Only Back-benchers can appeal to the Government. He is not a Back-bencher. I want to teach him!

**The Assistant Minister for Finance** (Mr. Keah): I can teach you better!

**The Temporary Deputy Speaker** (Mr. Wetangula): Order!

**Mr. Achieng-Oneko**: Mr. Temporary Speaker, Sir, is the hon. Keah not in order to express himself as a Member of Parliament?

**The Temporary Deputy Speaker** (Mr. Wetangula): Order! I think we shall all agree that Mr. Shikuku is not right!

**Mr. Shikuku**: He cannot do that!

**The Temporary Deputy Speaker** (Mr. Wetangula): Order Mr. Shikuku! You are now heckling!

**Mr. Nyagah**: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity.

Hon. Mudavadi has been commended by many people for the good work that he has done. We have also seen the calibre of Assistant Ministers he has; who tend to defend the Government. They spend very little time defending their own constituencies. God forbid if they will ever see the gates of this Parliament next time.

I would like to take on three or four Ministries that I would like to criticise. But before I do so, I know that we have been promised that development will be equitably distributed in this country. But according to the Estimates that we already have, that has not been the case. I would like to tell the Minister for Health that today I do not need to talk about health. I have talked about health on many occasions in the past and I think what I have been saying has fallen on deaf ears. Hon. Angatia has a big job to do in that Ministry.

I would like to take issue, firstly, with the Ministry of Local Government. It is unfortunate that the Minister for Local Government is not here. The first issue that I would like to raise with the Ministry of Local Government is the annexation of a whole location in Gachoka Constituency to become part of Embu Municipality. That happens to be a rural area and it is going to give more problems to an already existing municipality that has been unable to manage its own affairs. According to Cap. 265 of the Laws of Kenya, there are laid down regulations as on how an area can be annexed to become part of a municipality. The Ministry flouted the rules in annexing that location. I have consulted the people who were in the leadership at the time. The Minister for Local Government has persistently told this House that the rules were followed. A meeting of Embu leaders is scheduled to take place next week and one of the issues that we intend to tackle is that particular annexation of a whole location and placing it under a municipality, which is not benefiting them in any way other than raising the rates for water. Most people would normally fight for upgrading of their own areas, but in that case, we are fighting for downgrading of that area to be managed by the Embu County Council.

On the Ministry of Lands and Settlement, we have two locations where, 32 years after Independence, the people still live like aliens. They have not been given title deeds. The Minister for Lands and Settlement has categorically made a Statement in this House that within a year, title deeds will be given to the people of Kiambere, Makima and Karaba. A year later, this has not been experienced. I would like to appeal to the Minister for Lands and Settlement to be more committed to assurances that he gives to this House. We in Embu are looking forward to the day when we will be given our titles to those particular areas so that we can develop. How does a country develop? A country develops if, for instance, the citizens are able to use titles deeds that are issued to them. If title deeds are issued to the people of those two locations, they will be able to help the Government. As it is, it makes us remain as beggars. For how long are we going to remain like that?

Currently we have a Committee that has been appointed to look into the settlement of people in those two locations. We are appealing to the Government to, first of all, know that the settlement of people in the Mwea Settlement Scheme is not in dispute in Embu. We are asking Justice Chesoni and his team to listen to the views of the people of Embu. The Embu County Council has come up with a theory, and a practical one, as to how the settlement is going to be done. It has been pre-determined as to how that is going to be undertaken.

The Committee has gone round in neighbouring districts trying to get the views of the people there, but we would like to inform Justice Chesoni that, that particular area belongs to Embu. It is managed by Embu County Council and there is no dispute about that at all.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, if I may touch briefly on roads in Embu, most of the roads in tea growing areas have become impassable. We have, so far, been able to raise Kshs1.5 billion which ought to be distributed equitably into developing various parts of this country. As it is, part of the Kshs1.5 billion has gone to certain areas that do not necessarily need that money. Again, we appeal to the Minister concerned to ensure that the roads are graded equitably in Kenya. One wonders why we have a Provincial Works Officer in Embu. What role does he play if he is unable to look after some of the roads there? If you look at the Estimates, you will find that there is very little money that has been allocated for Embu. Most of it has, unfortunately, gone to certain districts. I think, in future, when it comes to Development Estimates, let us be more broad and recognise that Kenyan belongs to us all

and that we need to develop it as evenly as we can.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, if I may give a typical example, Embu District is one of them. Embu District has grown over the years. We have a sewerage problem that has been going on for a very long time. Looking through the Printed Estimates, I can see that Embu District has only been granted K£100,000. If I may look and compare it with an area in Uasin Gishu District, that is Eldoret Town alone, it has been allocated Kshs.1 billion through a grant by the Germany Government. It has also been given an extra Kshs332 millions to improve the sewerage system. Areas like Kisumu Town and Mombasa Town have not been taken care of, even as far as sewerage is concerned. The money is being channelled to one area. I do not want to discriminate or be seen as a tribalist but, for how long are we going to keep on developing the Rift Valley Province? They are taxpayers as we are. I have nothing against the people of that area, but I think when it comes to development, we must be more rational and decent in the manner in which we are going to take care of the resources.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, if I may touch on what everybody else has talked about; that is the Eldoret Airport, I do not want to be very critical. I just want to say that, every hon. Member has complained about the pathetic state of the roads where they come from, including hon. Keah. If only the Government was decent enough, it should be able to repair our roads. We have two international airports; the Moi International Airport at Mombasa and Jomo Kenyatta International Airport here in Nairobi. Those two airports are enough to carry out duties that are required. With an extra international airport coming up in Eldoret Town--- If part of that money was used develop our roads, there would be less hue and cry from hon. Members in this House. We would be able to develop those districts that are further and further away from Nairobi. That way, the Government would earn enough money. If we are able to get produce like coffee and tea on time for the outside markets, we would prosper.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I have looked very carefully at the Printed Estimates that we will soon be discussing in this House. I am surprised that most of the KANU Members of Parliament have been very critical of those Printed Estimates, but God knows what happens when they come to the day of reckoning; the day of voting, they vote as a block like sheep being led into a slaughter-house. History will judge many Members who sit in the back benches when they vote as a block. You are pulled overnight to come into the House and vote for the Government.

With those few words, I oppose the Motion.

**Bishop Tanui:** Bw. Naibu Spika wa muda, ningependa kuiunga mkono Hoja hii na kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kazi safi anayofanya. Tunasema ahsante sana. Nikirundi upande wa Kipkelion ambayo ni sehemu moja iliyosahaulika, nafikiri wakati Wizara ya Fedha inapokaa chini na kupanga mambo, ingeangalia Kipkelion na barabara ya kutoka Londiani mpaka Fort Ternan. Pesa zilitengwa za kurekebisha na kuweka lami barabara ya Londiani-Fort-Ternan, lakini zilihamishwa na kupelekwa kurekebisha barabara zingine. Barabara ya Londiani-Fort Ternan iliwachwa vile ilivyokuwa. Ningependa kusema kwamba sisi ni lazima tuseme ukweli uwe mchungu au mtamu. Nikiwa Mbunge wa sehemu hiyo, nitazidi kusema kwamba sisi wananchi wa Londiani tunaomba Serikali iangalie kwa makini barabara ya Londiani-Fort Ternan. Mhe. mwenzangu amesema kwamba Rift Valley imekuwa na maendeleo mengi sana. Ninashindwa ni Rift Valley gani anaongea juu yake kwa sababu ninatoka huko na hali Kipkelion yenyewe haina hata barabara za lami wala hospitali.

Bw. Naibu Spika wa muda, kituo cha matibabu cha Fort Ternan hakina vifaa vyo vyote na ningependa Waziri anayehusika, na pia Wizara ya Fedha pia, wakitengee pesa za kukiendeleza. Sasa hivi ninavyozungumza, katika hospitali ya Londiani, wananchi wanalazimika kutoa maji ya matumizi yao nyumbani. Naomba Wizara inayohusika ishughulike jambo hilo ili hospitali ya Londiani ipate maji. Kuna maji kwa wingi mjini lakini yameelekezwa kwa tajiri mmoja. Hupita karibu na hospitali hiyo. Katika hospitali hiyo, wananchi wanajibebea maji ya kutumia.

Bw. Naibu Spika wa muda, narudia kusema kwamba Mhe. mwenzangu ambaye, pamoja na wengine katika upande wa Upinzani, walisema kuwa uwanja wa ndege wa Eldoret haustahili kujengwa na wamekuwa na uchungu mwingi. Tunataka maendeleo katika Kenya nzima. Huu uwanja utafaidi Wakenya wote na tunauhitaji. Tunapongeza Serikali kwa kuujenga kwani ni faida kwetu. Tunazungumza kuhusu Eldoret Airport lakini hatuzungumzi kuhusu barabara za Mkoa wa Kati ambazo ni mbili mbili. Hata hayo ni maendeleo yetu zote. Lazima tuunge Serikali yetu mkono inapoendeleza sehemu yoyote katika nchi yetu.

Bw. Naibu Spika wa muda, lazima wafanyakazi wa Serikali wahakikishe kwamba wametumia pesa kwa njia safi. Wasizitumie kwa mahitaji yao kwani hata wakifanya hivyo kwa kujificha ni vibaya. Hata Musa alipokuwa akiwaongoza wana wa Israeli, ilifika wakati ambapo walimkosea Mungu. Naye Mungu aliwambia hawataiona nchi ya ahadi. Kwa hivyo, watumishi wa Serikali wanaombwa wafanye mema naye Mungu atawabariki wanapokuwa majumbani mwao.

Bw. Naibu wa Spika wa muda, sisi Wakenya tunafurahia uongozi mwema wa Mtukufu Rais Moi. Tunajua kuwa kila mmoja anataka kutawala lakini kwa sasa Rais Moi anaongoza vyema na tunamuomba Mungu amuongoze na amlinde.

Bw. Naibu Spika wa Muda, tumezungumza kuhusu pareto katika kiwanda kimoja huko Kipkelion. Kuna

miradi ambayo tumepitisha katika DDC lakini hakuna hata mradi mmoja umetekelezwa. Ningependa Mawaziri wote katika Kenya waende Kipkelion wanionyeshe ni mradi gani Kipkelion imepata. Hakuna maji, stima, lami, shule. Hakuna chochote ila tu Mungu. Ningependa kusema hivi: Kuna mradi moja ambao ulikuwa umepitishwa zamani, Kimalagit Water Project. Hata pesa za mradi huo zikatengwa na tukafurahi sana. Lakini baadaye, hatujui hizo pesa zilienda wapi. Kwa hivyo, nikisimama nikiwa Mbunge wa Kipkelion na tena nikiwa nimeokoka na ninampenda Yesu kama Mwokozi wetu, ningependa kusema kwamba wananchi wamepanda kahawa, lakini viwanda vya kupeleka kahawa hiyo hakuna. Hata barabara ya kuipitishia kahawa hiyo hakuna. Ukiangalia upande wa majani chai, mambo ni vile vile. Kwa hivyo, ningependa ndugu zangu na viongozi kama mimi kutoka upande wa Upinzani tuwe kitu kimoja na tuangalie nchi ya Kenya. Tujenge Kenya iwe kitu kimoja. Kama barabara ikitengezwa kutoka hapa hadi Kisumu tufurahi. Ikitengenezwa mpaka North-Eastern, tunafurahi. Barabara za sehemu zote zikitengezwa, tutafurahi. Najua kwamba ndugu zangu wakipiga kelele na kusema kwamba sehemu zao hazina barabara, wanajaribu kuficha kitu chochote. Msifiche kitu. Semeni haki na mtabarikiwa. Msipinge haki. Semeni haki na mtabarikiwa. Tukihesabu miradi ambayo imefanywa katika Mikoa ya Bonde la Ufa, Magharibi, Kati na Pwani, tutaona kwamba Mkoa wa Kati unachukua nafasi ya kwanza katika maendeleo. Hata tukiweka Mikoa ya Bonde la Ufa, Kaskazini Mshariki na Pwani pamoja, hatuwezi kupita Mkoa wa Kati kimaendeleo. Kwa hivyo, mshukuru na muendeleo namna hiyo. Kwa hivyo tungependa tuungane pamoja na tukae pamoja.

*[The Temporary Deputy Speaker*

*(Mr. Wetangula) left the Chair]*

*[Mr. Speaker resumed the Chair]*

Bw. Spika kuna jambo lingine ambalo ningependa kusema. Mimi nikiwa Mbunge, hii ni mara yangu ya tatu au ya pili kuliongea. Kuna kitu kimoja ambacho ningependa kulisema leo. Sisi tunatetea wananchi ambao walituchagua. Lazima tuwatetea kwa haki. Tuwatetea kwa kuungana mikono pamoja na kuunga Mtukufu Rais ambaye anaongoza nchi hii sasa mkono. Ukifanya mema Mungu atakubariki. Hujui siku moja utakuwa nani. Kwa hivyo tuungane pamoja. Ninawaunga mkono Mawaziri wote and wafanyakazi wa Serikali. Lakini wakifanya mabaya, nawambia katika Biblia Ufunuo 3:3 unasema, "Rudini nyumba---"

**Mr. Speaker:** Your time is up!

**Bishop Tanui:** Ahsante sana Bw. Spika.

**The Member for Machakos Town (Mr. Musyoki):** Ahsante sana, Bw. Spika kwa kunipatia nafasi hii, ili niweze kutoa hotuba yangu ya kwanza na pia nichangie Makadrio ya mwaka 1995/1996.

Bw. Spika, nawashukuru sana wenyeji wa Machakos Town walioniteuwa na kunichagua kama Mbunge wao kwa tikiti ya KANU. Pia nawashukuru marafiki zangu na viongozi wa KANU waliojiunga na mimi na kushirikiana pamoja wakati wa kampeini mpaka tukanyakua ushindi kwa tikiti ya KANU.

Nina masikitiko nikimtaja marehemu John Kyalo. Nikikumbuka vile amewafanyia wakaazi wa Machako Town maendeleo makubwa kupitia kwa Serikali tukufu ya KANU. Aliweza kuwafanyia miradi tofauti tofauti wakazi wa Machakos Town. Ushirikiano aliyowacha baina ya watu wa Machakos Town na Serikali ni mkubwa sana na natumaini kwamba ushirikiano wangu na wakazi wa Machakos Town utaendelea ili kuniwezesha kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo aliyacha bila kukamilika. Naomba kwamba huo ushirikiano na uhusiano uliokuwapo baina ya Marehemu, Serikali na wakaazi wa Machakos Town utaendelea. Ninaomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Pia nashukuru Serikali ya KANU tukufu ambayo inaongozwa na Mtukufu Rais Daniel Toroitich arap Moi kwa yale maendeleo na misaada imeweza kuwapatia wenyeji wa Machakos Town. Serikali iliwaisaidia watu wa Machakos Town na chakula wakati mgumu wa kiangazi kwa muda wa miaka miwili iliyopita.

Pia nashukuru Serikali ya KANU kwa ujenzi wa barabara. Imejengea wakazi wa Machakos Town barabara kutoka Makutano ya Mombasa-Nairobi hadi Jiji la Nairobi, na hata barabara ndogo ndogo ndani ya mji. Pia, kuna barabara inayoendelea kuwekwa lami kutoka mji wa Machakos Town hadi Kangundo. Hiyo ni shukrani kubwa sana. Nashukuru Serikali kwa mipango inayofanya ya kuendelea kuwasaidia watu wa Machakos Town.

Pia ninashukuru Serikali ya Mtukufu Rais kwa maji safi kutoka Kilimanjaro iliyowapatia watu wa Machakos. Sasa watu wa Machakos hawana shida ya maji kama hapo mbeleni. Hiyo ni shukrani kubwa sana.

Pia ningependa kumshukuru Waziri ya Afya kupitia Wizara yake kwa vile amewafanyia watu wa Machakos Town. Amewaletea dawa na anaendelea kufanya mengi kwa hospitali hiyo. Ni shukrani kubwa.

Pia, Bw. Spika, nashukuru Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri aliyoitoa kwa vile inaambatana na matakwa ya wananchi wa Kenya.

Kwa hayo machache ninaunga mkono Hoja hiyo.

**The Assistant Minister for Culture and Social Services (Mr. Kirior):** Bw. Spika, nakushukuru kwa

kunipatia nafasi hii kuchangia Bajeti hii ambayo ni nzuri.

Kwa kuchangia Bajeti hii, ningetaka kutaja shida mbali mbali ambazo zinatukabili huko nyumbani. Nataka kuongea juu ya maji. Huko Belgut, tumepitisha mradi mmoja wa maji. Kuna michoro mbali mbali na kila jambo limekuwa tayari kwa miaka 20. Lakini mpaka sasa, hatujapata maji hayo. Utekelezaji ndio bado kufanywa na huu ni mradi mmoja ambao unachukua theluthi mbili ya Belgut. Naiomba Wizara ya Ustawi wa Maji wafanye juhudi zao kuhakikisha kwamba maji hayo au mradi huo wa maji unatekelezwa. Ni jambo ambalo tumelizungumzia kwa miaka 20 tukitarajia kwamba maji haya yatakuja. Ni maombi yangu tupate maji hayo haraka iwezekanavyo. Naamini kwamba Wizara inayohusika itachukua hatua ifaayo.

Bw. Spika, tuna shida kubwa kwa mambo ya afya, hasa kwa madaktari ambao ni consultants, yaani wataalamu. Mara nyingi, watu wakienda huko wakitaka usaidizi, wanashauriwa waende katika hospitali za kibinafsi kama Aga Khan na kadhalika, ili wapate nafasi ya kutibiwa huko ili walipe pesa. Hawajui kwamba wagonjwa hao wana pesa ama hawana. Ni vizuri Wizara ya Afya ichukue hatua ifaayo kusimamisha jambo hilo la private practice kwa sababu limewaumiza watu wengi sana. Hata juzi, nilimwona mtu mmoja ambaye alishauriwa aende Aga Khan ambapo alitakiwa atoe au alipe kiasi cha KSh.100,000.00 kwa matibabu. Yule ambaye anatoa agizo hilo ama yule ambaye anamshauri ni daktari ambaye anafanyia kazi Serikali. Tunasikia wengi ambao wanafanya namna hiyo. Hilo ni jambo la kuudhi sana. Ni vizuri Serikali iongeze mshahara wa madaktari halafu haya mambo ya private practice yafungwe. Ama daktari aache kazi ya Serikali aende ajisimamie. Hiyo ni bora kabisa kuliko daktari kutumia vifaa vya Serikali kutibu mtu halafu apate pesa. Jambo hili limeleta taabu nyingi sana. Naamini kwamba Waziri anayehusika atachukua hatua kurekebisha jambo hilo ili daktari akiwa mfanyakazi wa Serikali, aache mambo ya private practice. Lakini jambo muhimu ni kuangalia ni mambo ya mshahara kwa sababu daktari anaweza kutibu mgonjwa mmoja na kupata pesa ambazo ni zaidi ya mshahara wake wa mwezi.

Jambo lingine, Bw. Spika, ambalo tumeona kwa hospitali nyingi ni kuhusu mambo ya mortuary, yaani chumba cha kuhifadhi maiti. Mtu anapofariki, jamaa yake wakitaka kuchukua maiti, mara nyingi wale wafanyakazi wa huko mortuary wanasumbua watu sana kwa sababu wanataka hongo. Sasa, mtu analia kwa ajili ya kupoteza mtu wake halafu anasumbuliwa kwa sababu ya hongo kwa sababu wanajua ni shida kwa mtu kwenda kutoa ile maiti. Yafaa Wizara ichunguze jambo hilo na likomeshwe kabisa, ili jamaa ya marehemu wanapokwenda kuchukua maiti, wasaidiwe na wasisumbuliwe na wafanyakazi hao wa mortuary. Tumetaabika sana kutokana na jambo hili ambalo linahusu hospitali nyingi sana.

Kwa upande wa kilimo, Bw. Spika, kilimo ni muhimu kwetu katika nchi hii ya Kenya. Lakini kuna mambo machache ambayo nataka yarekebishwe. Katika Muhoroni Sugar Factory, nataka kutoa shukrani kwao kwa sababu kwa wakati huu wamejaribu kusimamia vizuri wakulima wa miwa na wanalipwa vizuri. Lakini jambo ambalo sisi kwa upande wa Kericho tunalalamikia na kusikitikia ni kuhusu waajiri wa wafanyakazi katika kiwanda hicho. Sisi katika upande wa Kericho tunatoa nusu ya miwa ambayo inapeleka Muhoroni Factory lakini ukiangalia uajiri wa wafanyakazi katika kiwanda hicho, wale watu kutoka upande wa Kericho si zaidi ya watu 30 kwa watu zaidi ya 2,000 ambao wanafanya kazi huko. Tunalalamika kwa sababu tunataka usawa wa kazi. Sisi pia tunasaidia kiwanda hicho. Tunachukua miwa yetu huko lakini ikija upande wa uajiri hatupati nafasi iliyo sawa na wenzetu wengine. Ukienda huko Kericho utasikia malalamiko yetu ndio hayo. Ulipaji wa wakulima ni sawa kwa wakati huu lakini tuna shida kwa upande wa uajiri wa wafanyakazi. Tunataka uajiri sawa ili zote tufaidike kwa sababu tunapeleka miwa yetu huko.

Bw. Spika, kuna jambo ambalo mhe. Prof. Ouma alitaja kuhusu mambo ya kemikali ambayo inamwagwa kwa maji. Muhoroni Sugar Factory pamoja na Agro-Chemical wanamwaga maji ya sumu katika mto Kipchorian; upande wa Kisumu unaitwa Nyando. Maji haya yameleta maafa kwa ng'ombe, samaki na kadhalika. Kwa hivyo, nataka Muhoroni na Agro-Chemical watafute mahali pengine pa kumwaga sumu hiyo lakini wasimwage kwa mto. Sisi pamoja na wanyama tunapata maji ya kunywa katika mto huo. Kwa hivyo, ni taabu kama wanaweka sumu kwa maji hayo. Inakuwa ni hatari kwa kila kiumbe. Tunaomba warekebishe jambo hilo.

Jambo lingine, Bw. Spika, kuhusu kilimo ni mambo ya cess ama kodi. Tunajua cess inachukuliwa kwa mimea mbali mbali. Cess ya majani chai inasimamiwa na kamati maalum ambayo ilibuniwa. Lakini cess kwa mimea mingine inaachiwa makonseli. Sijui ni kwa nini cess zote hazikuachiwa kamati hiyo maalum ikiwa wafanya kazi zaidi kuliko makonseli. Ingefaa waachiwe wasimamie zote ama si hivyo makonseli wasimamie zote. Sijui ni kwa nini kuna vyama viwili ambavyo vinasimamia cess zote ambazo zinahusu wakulima wetu.

Bw. Spika, jambo lingine ambalo ningetaka kugusia ni kuhusu mambo ya mbegu za mahindi. Mwaka huu, mahindi kwetu si nzuri na ukichunguza sana, utapata kwamba kuna ujanja fulani; hatukupata mbegu sawa. Hata ile dawa ya kuweka kwa mahindi, pia si sawa.

Hata ile dawa inayotiwa kwa mahindi haiwi wadudu. Inaonekana kuna watu walaghai ambao wamechanganya dawa kiasi kidogo na kitu kingine. Tumeona kuwa ukiyaweka mahindi dawa hiyo na kuyaweka katika gunia, baada ya muda mfupi, mahindi hayo yatakuwa yameliwa na wadudu. Inafaa Wizara ichunguze jambo hilo ambalo linawaletea

wakulima hasara na hali uchumi wa nchi hii unategemea ukulima.

Jambo lingine ni kuhusu watu ambao wanastaafu kazi zao. Inafaa Serikali iwalipe maofisa wanaostaafu pesa zao mara moja. Mara nyingi tunawaona watu waliostaafu wakitaabika hapa Nairobi sana, wakiendelea kufuata malipo yao na huku wanaendelea kuambiwa waje kesho.

**Mrs. Ngilu:** Thank you, Mr. Speaker, Sir. I wish to limit my contribution on the Budget to the question of poverty alleviation.

First of all, I would like to congratulate the Minister for Finance for specially setting aside K£377 million - the equivalent of about Kshs7.5 billion - for poverty stricken Kenyans. I am also happy to note that this figure will be tripled in the next three years. This plan to progressively triple the figure of K£377 million over a period of three years is in keeping with the President's promise during the last year's national conference on social dimension of development, which was held at the Kenyatta International Conference Centre. It is also in keeping with the theme of alleviating poverty echoed in Copenhagen in March, 1995, during the world's social summit on development. I am also pleased because I participated in that conference and what we undertook to do for this country seems to be bearing fruits.

However, while that sounds very good at the theoretical level, the administration of those funds will be very crucial in measuring what the Government can do for the poor in this country. In my view, there is an urgent and important need to do proper planning for that money. Emphasis should be put on vocational training for youth and women, who are the target groups. That will enable them to have proper understanding of their needs and solve their own problems.

I do not believe in the promises being sung every day that people in Kanu zones will get development. I come from a non-Kanu zone, but I am sorry for my counterparts who are in Kanu zones because their areas are worse than mine. That promise, which is given every now and then to defectors, should cease because it does not help anybody in this country. I think all Kenyans, whether they are in Kanu or in the Opposition, are suffering equally. It is high time that we all understood the need to alleviate poverty in the whole country. It is for all of us to take upon our shoulders, irrespective of our party affiliations, the responsibility of making use of the funds that have been made available by the Minister to help our own people.

To that end, I would like to see proper emphasis put on basic training in areas like accountancy, book-keeping and access to savings and credit. That is the only thing that can provide the impetus for sustainable development. I say that because the current banks that offer credit and saving schemes to Kenyans would not suffice where ordinary mwananchi has little money. The current banks are elitist and are not suitable for running the projects of the poor. They are profit oriented and charge high interest rates and ledger fees. Women and the youth, who sell their merchandise along road sides and within parks, will not get any assistance from commercial banks. Therefore, the Co-operative Bank of Kenya and the co-operative societies should now take up the opportunity of offering services to the rural poor, so that women with little money and small businesses can have a place to keep their money. For instance, a woman who works and makes Kshs200 in a day might want to save Kshs100, but she will not be able to save it since even opening a bank account in most commercial banks needs between Kshs3,000 and Kshs5,000. Therefore, such a woman has no way of saving something for the future needs of her family.

In the actual implementation of the projects, we need to avoid a situation of misappropriation, misapplication and misuse or outright theft of the funds meant for the poor. Proper committees should be set up from the local to the national level. I suggest that a proper system where qualified, competent, honest, experienced and non-partisan local people could be put in place to identify the people who should benefit from those funds. I would like to hereby recommend women to be the majority in the membership of the committees that I am suggesting. That is because, as we know, women have been known to have less appetite for the shilling.

Mr. Speaker, Sir, I hope that this time round, the Minister is not going to fall into the well known trap of the World Bank, the IMF, international donor community and the non-governmental organisations that operate in our country. That kind of money may be diverted from the targeted poor and may be put into endless researches, meaningless seminars, cocktails, luncheons and luxurious travelling, which will take 75 per cent of the funds, so that the money never reaches the rural poor. That has been happening and I hope hon. Members will find time to read a book entitled "Lords of Poverty" by Graham Hancock. It so clearly spells out how money that is intended for the poor is spent by the people who give it out. We do not have to do any more research to find out how poor people in this country are. That has been done. For instance, we are about to go for the Beijing Conference. I, as a Member of Parliament, will have to spend an enormous Kshs250,000. Surely, what poverty am I going to discuss in Beijing when I know it here? That Kshs250,000 is enough to build three good dams for my constituency and women will farm their own food and will, at least, be able to alleviate their poverty and get out of most of the problems that they are experiencing today.

Mr. Speaker, Sir, my last point would be the issue of tax relief. The Minister will never get away with this.

He showed open discrimination on that when he gave a higher tax relief to married men. We know the burden of looking after a family. The burden of an African family lies squarely on the shoulders of a woman. Surely, what criteria did the Minister use to give higher tax relief to men and not to women, when we know that, today, most households are run by women?

I beg to support.

**The Assistant Minister for Land Reclamation, Regional and Water Development** (Mr. Chepkok): Ahsante sana, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili niungane na wenzangu kwa kuzungumzia Bajeti ambayo ilisomwa na Waziri juzi.

Bajeti hiyo ilikuwa nzuri sana kwa raia, isipokuwa kitu kimoja ambacho hata mimi sikukubaliana nacho. Ni mambo ya kuruhusu uagizaji wa mahindi kutoka nje. Bei ya mahindi ambayo wananchi wanalima itashuka. Hiyo itakuwa ni shida sana kwa wakulima. Bei za mbolea na madawa zinapanda na bei ya mahindi inashuka. Hiyo inaumiza mkulima. Mwaka ujao, kutakuwa na shida kwa sababu mwaka huu, watu wengi hawajapanda mahindi kwa sababu ya kukosa kulipwa na NCPB pesa ambayo wangetumia kununua mbegu na mbolea. Kwa hivyo, mwaka huu, watu wachache ndiyo walipanda mahindi. Hiyo ndiyo sababu ninaomba Serikali ichunguze kwa makini swala la uagizaji wa chakula kutoka nje.

Bw. Spika, nakubaliana na mwenzangu, mhe. Ngilu, kwa yale ambayo amesema kuhusiana na mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs) kwa sababu ni ukweli. Mara nyingi, zile pesa ambazo hutolewa na mashirika hayo hutumiwa kwa masemina na kulisha watu mahotelini. Nyinyi mnakuja kulishwa hapa na kula hotelini, lakini raia ambao wako nyumbani wanangoja pesa kwa sababu wana shida kubwa sana. Tumeona visa vingi sana vya aina hiyo.

Hata kwangu, nimeona watu wakipelekwa kwa semina, na wanatumia zaidi ya shilingi milioni tano. Yule mama ambaye anatoka katika lokesheni fulani amefunzwa kweli, lakini hakuna kitu ambacho anaenda kufanya. Mimi naona huo ni wizi. Afadhali mtu atuambie ya kwamba tumepata pesa kutoka kwa wafadhili ambayo itafaidi watu. Kama kuna mradi wa maji, raia mwenyewe aende kununua vile vitu ambavyo vinahitajika kwa ujenzi wa mradi huo. Akipewa LPO, mwenyewe atachunga pesa hizo. Lakini tukiwapatia maafisa, wengi wao huiba. Unakuta kwamba afisa anadai "night out allowance", na hali haendi mbali. Anadai "night out allowance" ya karibu shilingi 5,000, na kumbe amelala kwake. Kwa hivyo, mimi nauliza Serikali iwapatia wananchi wenyewe pesa hizo. Kama mradi unagarimu shilingi milioni tano, raia wenyewe walio kwa kamati tekelezi wapewe nafasi ya kuchunga hiyo pesa na watekeleze mradi huo wenyewe. Itakuwa rahisi kwao kuchunga pesa yao kuliko maafisa wa Serikali. Wizi umekuwa mwingi sana katika Serikali. Hilo si jambo la kuficha. Tumeona wengi.

Hata Jumatatu, nilikuwa katika mkutano wa DDC, na tuliambiwa jambo la ajabu sana kuhusu daktari mmoja katika hospitali ya Iten. Kuna mama mmoja mja mzito ambaye aliletwa hospitalini usiku. Badala ya huyo daktari kumfanyia upasuaji, alisema: "Wacha ikae mpaka kesho". Huyu mama aliaga dunia usiku bila kusaidiwa, na huyo daktari alikuwa anakunywa tu, akitumia zile pesa alizokuwa amepata kwa kuuza madawa. Hiyo ni ajabu sana! Hilo ni jambo ambalo sisi wote katika Serikali na Upinzani tunapaswa kupinga. Tusiwe watu wa kuunga mkono tu, na huku watu wanamalizika. Hatuwezi kukubaliana na mambo kama hayo. Hata Mtukufu Rais anapinga mambo kama hayo. Yeye analia kila siku, na sisi wenyewe tumeanza kutia fitina huko, tukisema yawaachiliwe. Lakini ni lazima sisi zote katika Serikali na Upinzani tuungane pamoja kupinga wizi ambao umefika katika Kenya. Tusipofanya hivyo, basi, ndungu zanguni, poleni sana. Tukitaka kuja kwa Bunge hili tena, ni lazima tuonyeshe raia kwamba, ijapokuwa ni chama gani cha kisiasa tunachounga mkono, tuko pamoja na tunataka kujenga nchi hii. Si kupigana tu na mhe. Shikuku hapa, na tukitoka hapa, tunaenda kunywa chai pamoja na yeye, tukizungumza mambo mengine. Raia huko nje wanaachwa wakisema: "Aah, hawa walipigana leo!" Lakini huko nje, tunakunywa chai pamoja, tukizungumza mambo mengine. Ni lazima raia wajue kwamba tuko pamoja na tunajenga Kenya. Chama cha kisiasa ni nini? Tusipokaa pamoja, wewe utaendelea kurukaruka hapa ukisema "KANU itatawala kwa miaka 200". Wakati huo, sisi hatutakuwa hapa. Tutakuwa tumeenda. Ndiyo sababu mimi nawambia kwamba tuungane ili tujenge nchi hii.

Nafikiri hata rafiki yangu, mhe. Kibaki, alifanya makosa sana kuingia katika Upinzani. Angebaki kwa KANU kwa sababu KANU itatawala kwa miaka 200 ijayo, lakini tujenge nchi hii. Tujenge tukiwa pamoja, na tukiwa katika Bunge hili, turekebishe yale mabaya ambayo yamefanyika. Hicho ndicho kitu kimoja ambacho mimi ningemba. Tusitukanane. Hautafaidika kwa kutukana mwenzako. Hata ukitumia magazeti kutukana mwenzako, hakuna kitu utafaidika nacho hapo. Yako ni kwenda kwa magazeti ili ujulikane. Unazungumza nini? Wengi wenu hapa hamwendi nyumbani kwenu.

*(Mr. Chepkok hit the Table with his fist)*

Munashinda hapa Bungeni; hamwendi nyumbani kwenu.

